TANGAZO LA SERIKALI NA. 585 la tarehe 18/9/2023

SHERIA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 272)

_____

AMRI

_____

(Imetolewa chini ya kifungu cha 29 (1)(d))

AMRI YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA SUMBAWANGA (SUMBAWANGA WSSA) YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira za Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga (Sumbawanga WSSA) ya mwaka 2023.

Marekebisho ya bei

2. Bei za Sumbawanga WSSA zinarekebishwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Masharti

3. Ushuru ulioidhinishwa utazingatia masharti yafuatayo:

(a) Mnamo au kabla ya tarehe 30 Septemba 2023, Sumbawanga WSSA itawasilisha Mpango wa Biashara uliorekebishwa ambao utajumuisha bei zilizoidhinishwa na mpango kazi wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(b) Kabla ya kutolewa kwa Ankara kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa, Sumbawanga WSSA itatoa ushahidi kwa EWURA kwamba imewataarifu wateja wake juu ya amri ya ushuru na imetoa uelewa wa kina kwa wadau wake wakiwemo wateja, viongozi wa serikali,

kisiasa na wawakilishi wa dini;

(c) Mnamo au kabla ya tarehe 31 Desemba 2023, Sumbawanga WSSA itawasilisha deni lake la tozo ya udhibiti iliyobaki ya TZS 62,087,694.23 kwa Kumbukumbu za tarehe 21 Juni 2023. Baada ya hapo, Sumbawanga WSSA itazingatia mahitaji ya tozo ya udhibiti kwa kuwasilisha tozo hizo kwa wakati;

(d) Sumbawanga WSSA itatekeleza miradi kwa kutumia fedha zinazotokana na ushuru, tozo na ada kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Pili;

(e) Sumbawanga WSSA itafikia viashiria muhimu vya utendaji kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali la Tatu;

(f) Sumbawanga WSSA katika kipindi cha kila mwaka itawasilisha kwa EWURA taarifa za masharti ya utaratibu wa ushuru wa forodha na gharama ya mahitaji ya mapato kama yalivyoonyeshwa kwenye Jedwali la Nne kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji;

(g) Katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji unaendelea hasa wakati wa kiangazi, Sumbawanga WSSA itaandaa na kutekeleza mpango wa kuvuna maji ya mvua;

(h) Ifikapo tarehe 30 Juni 2026, Sumbawanga WSSA itafanya ukaguzi wa ufanisi wa utekelezaji wa Mpango wa Biashara kwa mujibu wa Kanuni ya 18 ya Kanuni za Usambazaji wa Maji safi na Usafi wa Mazingira Leseni na Ubora wa Huduma za mwaka 2020 na kuwasilisha taarifa kwa EWURA; na

TS Na. 849 ya 2020

(i) Sumbawanga WSSA itaendelea kuipatia EWURA taarifa kuhusu hali yake ya fedha na uendeshaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA

kufanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka hiyo ikilinganishwa na mamlaka nyingine za maji safi na usafi wa mazingira na uboreshaji wa utendaji wake kwa muda;

Kufutwa kwa TS. Namba 256 ya 2020.

4. Amri ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga ("Sumbawanga WSSA") (Marekebisho ya Ushuru wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira), 2020 inafutwa.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): bei za maji za sasa na zilizoidhinishwa

Kundi la Wateja	Matumizi (m^3)	Kipimo	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa		
			2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
Majumbani	0-5	Sh./Mita ya Ujazo	1,000	1,563	1,594	1,615
	Zaidi ya 5		1,245			
Taasisi			1,280	1782	1817	1841
Biashara			1,280	1,790	1,820	1,850
Viwanda			1,480	2,060	2,101	2,129
Magati		Sh./Lita 20	20	30	30	30
Wastani			1,146	1,596	1,627	1,649

Jedwali Namba 1(b): ada za sasa na zilizoidhinishwa kwa maunganisho mapya ya maji (Shilingi kwa maunganisho)

Kundi la wateja	Ada ya sasa	Ada iliyoidhinishwa		
	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
Majumbani	Asilimia 20 ya gharama za maunganisho kama ilivyoainishwa kwenye kanuni ya	26,000	26,000	26,000
Taasisi		26,000	26,000	26,000
Biashara		26,000	26,000	26,000
Viwanda		26,000	26,000	26,000

Kundi la wateja	Ada ya sasa	Ada iliyoidhinishwa		
	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
	26 ya Kanuni za Maji za mwaka 2019			

Jedwali Namba 1(c): Tozo za sasa na zilizoidhinishwa za kurejeshewa huduma ya maji (Shilingi kwa marejesho)

Kundi la wateja	Tozo ya sasa	Tozo zilizoidhinishwa		
	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
Majumbani	15,000	15,000	15,000	15,000
Taasisi	15,000	15,000	15,000	15,000
Biashara	15,000	15,000	15,000	15,000
Viwanda	15,000	15,000	15,000	15,000

Jedwali Namba 1(d): Tozo za sasa na zilizoidhinishwa za uondoaji wa majitaka (Shilingi kwa tripu)

Kundi la wateja	Tozo ya sasa	Tozo zilizoidhinishwa		
	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
Majumbani	80,000	90,000	100,000	120,000
Taasisi	90,000	120,000	130,000	150,000
Biashara	90,000	120,000	130,000	150,000
Viwanda	100,000	120,000	130,000	150,000

Jedwali Namba 1(e): Tozo za Sasa na zilizoidhinishwa za kumwaga majitaka kwenye Mabwawa ya Sumbawanga WSSA (Shilingi Kwa Tripu)

Kundi la wateja	Tozo ya sasa	Tozo zilizoidhinishwa		
	2022/23	2023/24	2024/25	2025/26
Majumbani	20,000	20,000	20,000	20,000
Taasisi	25,000	20,000	20,000	20,000
Biashara	35,000	20,000	20,000	20,000

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(d))

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

Kazi itakayofanyika	Kiasi (Shilingi Milioni)		
	2023/24	2024/25	2025/26
Kununua dira za maji 6000 (dira 3000 mwaka 2023/24 na dira 3000 mwaka 2024/25)	127	131	
Kununua na kufunga dira za maji 4500 kwa ajili ya wateja wasio na (dira 2000 mwaka 2023/24 na dira 2,500 mwaka 2024/25)	67	119	
Kununua dira za maji mengi 28 kwa ajili ya machujio ya maji ya Majengo, Senga na Kizwite na Matangi ya Katandala na Kizwite	19		
Kununua dira za maji mengi 22 kwa ajili ya Block KK DMA, Makutano DMA, Kasisiwe & Osterbay DMA, Sokolo DMA, Karitus-Katandala DMA, Mzee Shirima NHC DMA, Bangwe DMA, New Holand DMA na Senti & Mji Mwema DMA			15
Kununua 200m HDPE DN 355, PE 100 PN 16 na viungio vyake kwa ajili ya bomba la Kaloleni (Kolongoni), Kukarabati kilometa 6 za mtandao wa maji ifikapo Juni 2024 , Kilometa 17 ifikapo Juni 2025 na kilometa 22 ifikapo Juni 2026 katika maeneo ya Jangwani,Mazwi, Majengo na Kasisiwe	8	20	38
Kununua/kukarabati pampu ya umeme, mota ya umeme na *Soft Starter* ifikapo Juni 2025 kwa ajili ya kituo cha kusukuma maji cha Old Kaswepepe		80	
Kukarabati SCADA na PLC kwa ajili ya vituo vya kusukuma maji na visima ifikapo 2025	-	20	-
Kununua vali 19 ifikapo Juni 2024, *Electromagnetic Digital Flow* 19, mota 5 ifikapo Juni 2025, Kununua pampu 2 zenye mota ifikapo Juni 2026	75	100	152

Kununua na kufunga dira za kidijitali kwa ajili ya maingizo na matoleo ya maji katika tangi la Kaswepepe na kituo cha kusukuma maji cha Katandala ifikapo Juni 2024, Kununua na kufunga dira za kidijitali kwa ajili ya tangi la Kilimani ifikapo Juni 2025, na Kununua na kufunga dira za kidijitali kwa ajili ya matangi la Katandala Tank na Old Katandala ifikapo Juni 2026	75	70	103
Kuongeza mtandao wa usambazaji wa maji kwa kilometa 66 mwaka 2024/25 na kilometa 34 mwaka 2025/26		1,010	540
Kukarabati machujio ya Majengo, Kizwite, na Senga	45	60	150
Kununua 30KW VFD kwa ajili ya kisima Na.5 ifikapo Juni 2024, Kununua 25KW VFD kwa ajili ya visima Na.80 na 81 ifikapo Juni 2025 na kununua 27KW VFD kwa ajili ya visima Na.23 na 15 ifikapo Juni 2026	15	15	30
Kukarabati mabomba ya kusambaza maji kwa kilometa 22 mwaka 2023/24, kilometer 34 mwaka 2024/25 na kilometa 34 mwaka 2025/26 katika maeneo ya Izia kilomita10, Jangwani kilomita 30, Mazwi kilomita 20, Majengo kilomita 20, Sumbawanga Asili na Edeni kilomita 10	150	150	150
Kukarabati tangi la Old Makao Makuu Tank Ifikapo Juni 2024/25		100	
Kujenga uzio eneo la tangi la Kilimani lenye ukubwa wa 2.7 ha	10	25	10
Kujenga uzio eneo la tangi la Sokolo lenye ukubwa wa 3.8 ha	20	30	20
Kujenga uzio eneo la tangi la Kizwite lenye ukubwa wa 2.9 ha	15	20	15
Kujenga uzio eneo la tangi la Kaswepepe lenye ukubwa wa 4.0 ha	20	25	20
Kujenga uzio eneo la tangi la Kafurusu lenye ukubwa wa 2.2 ha	20	22	20
Kujenga uzio eneo la tangi la Majumbasita lenye ukubwa wa 2.7 ha	15	28	15
Kukarabati visima viwili mwaka 2023/24, vitatu mwaka 2024/25 na vitatu mwaka 2025/26	50	50	50
Kukarabati jengo la ofisi ifikapo Juni 2024	75		
Kununua pikipiki nne ifikapo Juni 2026		14	14

Kununua gari jipya moja mwaka 2024/25 na gari jipya moja mwaka 2025/26		150	90
Kununua magari mapya mawili mwaka 2023/24 na magari mapya matatu mwaka 2025/26	10	-	14
Kununua magari mapya mawili ifikapo Juni 2025 na gari moja ifikapo Juni 2026		180	90
Kununua kompyuta mpya nne ifikapo Juni 2026		6	6
Kununua kompyuta mpya 4 mwaka 2023/24, kompyuta 4 mwaka 2024/25 na kompyuta 4 mwaka 2025/26	12	12	12
Kukarabati matekeo ya Ndua, Mwambazi, Momoka na Muva ifikapo Juni 2026	10	25	30
Kununua samani mpya za ofisi ifikapo Juni 2026		30	30
TOTAL	870	2,530	1,634

JEDWALI LA TATU

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(e))

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

Maelezo	Kizio	Lengo la Utendaji		
		2023/24	2024/25	2025/26
Wananchi wanaoptata majisafi	%	88	92	95
Upotevu wa Maji	%	27%	22%	20%
Kiwango cha Kufunga Dira za Maji kwa Wateja	%	100	100	100
Ufanisi katika Ukusanyaji wa Mapato	%	98	98	99
Viwango vya ubora wa maji	%	100	100	100

JEDWALI LA NNE

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(f))

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA

Maelezo	Kiasi (Shilingi Milioni)		
	2023/24	2024/25	2025/26
Gharama za uzalishaji	832.72	874.70	903.14
Gharama za usambazaji	46.86	49.20	51.66
Gharama za matengenezo	270.00	286.00	305.00
Malipo ya wafanyakazi	1,306.38	1,463.63	1,496.50
Gharama za Ofisi	703.79	751.56	788.07
Gharama za usafi wa Mazingira	33.81	35.50	37.28
Matangazo ya biashara	53.04	98.20	58.48
Matukio na michango	18.96	21.98	23.17
Gharama za Benki	1.45	1.52	1.60
Jumla ya gharama za uendeshaji	3,267.02	3,582.29	3,664.89
Uchakavu wa mali na miundombinu	1,370.30	1,536.53	1,729.51
Faida ya uwekezaji	11.76	12.89	12.88
Mapato jumla yanayohitajika	4,649.08	5,131.71	5,407.27
Ondoa: Tozo za huduma ya Majitaka	58.75	31.33	36.79
Ada za Maunganisho Mapya ya Maji	39.00	39.00	39.00
Ada za Kurejeshewa Huduma	29.79	26.54	24.36
Mapato Mengine ya Biashara	15.07	15.22	15.38
Faini za Maunganisho Yasiyo halali	16.29	16.29	16.29
Mapato Kutokana na Mauzo ya Maji	4,490.18	5,003.33	5,275.46

Dodoma,
……..., 2023

JAMES A. MWAINYEKULE
Mkurugenzi Mkuu